Changamoto ya Biblia kwa Mzazi na Mtoto

Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee. – Mithali 22:6

Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na uyanene uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo… – Kumbukumbu 6:5-7

"Nataka watoto wangu waijue Biblia," ni kauli ya msisitizo ambayo wachungaji na walimu Wakristo husikia ikisemwa majumbani. Tunapenda kuyajua maandiko, na tunataka watoto wetu wayajue maandiko pia. Ikiwa wewe una umtazamo huu, basi jiunge na Changamoto ya Biblia ili nyumba yako iwe ya wasomaji wa Biblia.

Kwa kawaida kanisa lina masaa 40 tu katika kila mwaka ili kubadili maisha ya mtoto. Mzazi katika hali ya kawaida ana masaa 3,000 kwa mwaka ili kubadilisha maisha ya mtoto. Fikiri jambo hili. Wewe ndiye mtu anayeweza kubadili maisha ya mtoto wako kuliko mwingine yeyote. Zawadi ya muda wako itawajengea watoto wako kujiamini na imani kwa Mungu. Kama una kanisa zuri, unahitaji msaada wake, kutiwa moyo na utaalamu wake ili kukusaidia wewe kuwa mtu wa kwanza kuleta mabadiliko katika maisha ya mtoto wako. Lakini pasipo moyo wa kujituma na usikivu, kanisa linaweza kufanya kidogo sana ili kuleta mabadiliko ya kiroho katika maisha ya mtoto wako.

Utafiti wa nyumba ambazo huhudhuria kanisani mara kwa mara uligundua kwamba ni wazazi wachache hujadili mambo ya kiroho na watoto wao. Katika utafiti mwingine uliyohusisha watu 80,000, 87% wanadai kuwa kuna umuhimu mkubwa kuifahamu Biblia. Katika Biblia Mungu anatumia familia kama njia ya kuelezea habari ya upendo, msamaha, mapatano na uponyaji. Biblia ni habari ihusuyo familia ya Mungu. Kwa pamoja, kama kanisa na familia, tunakualika kujifunza kusoma Biblia na mtoto wako au watoto wako ili uonekana mbele za Mungu kuwa ni mmojawapo wa watu wa Mungu, waliobadilishwa na wanaopenda kufanya kazi ya Mungu.

Lengo la Changamoto ya Biblia kwa Mzazi na Mtoto ni:

- Kualika familia ili kujihusisha kikamilfu katika Changamoto ya Biblia
- Kuchunguza jinsi kanisa linavyoweza kusaidia familia kusoma Biblia inayofaa kwa kuzingatia umri
- Kushirikiana kuhakikisha kwamba kanisa na familia vinakuwa pamoja na kuimarishwa katika uhusiano na Mungu kupitia usomaji wa Biblia wa mara kwa mara.

Kusoma na kujifunza Biblia pamoja kama familia huleta matokeo yafuatayo:

- Husaidia familia kukuza mahusiano
- Hufungua milango ya mahusiano
- Husaidia watoto kujua kuwa matendo ya imani huanzia nyumbani.
- Hubadilisha maisha yetu kila siku na kwa wakati wote.

Basi tushirikiane na kugundua jinsi Changamoto ya Biblia inavyoweza kutenda kazi katika nyumba yako. Tungependa kusikia kutoka kwako. Tufahamishe ikiwa ungependa kushirikiana nasi kwa kututembelea katika tovuti hii: www.thecenterforbiblicalstudies.org na kujiunga kuwa mshiriki wa Changamoto ya Biblia kwa Wazazi na Watoto.

Siyo muda mrefu, nyumba moja walitushirikisha kuwa wangependa sana kujenga maisha yao katika msingi wa Neno la Mungu. Hata hivyo, walihitaji muongozo zaidi. Pasipo muongozo, ni kama kipofu anamuongoza kipofu. Watoto wetu hutufundisha mengi kwa kadri tunavyoshirikiana pamoja. Wanataka kuijua Biblia. Hivyo, kwa nini tusijifunze pamoja nao.

Tunawezaje kusoma Biblia kama familia?

Hapa kuna hatua kadha za kuwasaidia watoto wetu katika Changamoto ya Biblia ambayo inaweza kutusaidia na sisi pia:

1. Chagua habari ya Biblia iliyo nyepesi kuisoma – kuna Biblia nyingi za kuchagua zilizopo maalum kwa ajili ya watoto, ambazo zinaweza kueleweka zaidi kwa watoto kuliko zile za watu wazima tulizozizoea.

- **Soma Biblia ya Masimulizi ya Mvuto, iitwayo *The Spark Story Bible***

Biblia hii ya watoto yafaa sana kwa wenye umri wa miaka miwili hadi wale wa darasa la pili. Kitabu hiki cha masimulizi kina vielelezo vizuri, theologia nzuri, kinavutia na kinaamsha mawazo. Ndugu Squiggles anaunda vema kila simulizi na kuvuta usikivu wa watoto. *The Spark Story Bible* humvutia msomaji na yule anayesikiliza pia kwa kuuliza maswali na kutoa mambo ya kufanya. Huelezea masimulizi muhimu ya Biblia ambayo yanaweza kupendwa na watoto na huacha masimulizi ambayo yasiyopendwa na waoto. Tembelea tovuti hii: www.sparkbibles.org

- **Soma 'Kitabu cha Masimulizi kwa Watoto', yaani *The Story for Kids***

Mfululizo huu wa mkusanyiko wa masimulizi ya Biblia uliyochapishwa na Zondervan umeunganishwa pamoja katika mtindo wa masimulizi marefu mithili ya kitabu cha watoto. Sehemu za Biblia zinazojirudiarudia na kuchosha zimeachwa kabisa. Pia kuna toleo la kitabu kama hiki linalofaa kwa watu wazima na linaitwa *The Story*, yaani 'Masimulizi', ambayo yafaa sana kusomwa na mzazi yoyote. Baada ya kusoma 'Kitabu cha Masimulizi kwa Watoto', wewe na motto wako mtakuwa mmepata uelewa mzuri zaidi wa Biblia. Tembelea tovuti hii: www.thestory.com ili kuagiza nakala.

- **Soma 'Biblia ya Watoto ya Kina Kirefu', yaani *Deep Blue Kids Bible***

Tunapendekeza toleo hili la Biblia ya Kiingereza cha Kisasa ambayo inafaa kwa wenye umri wa miaka 7 hadi 12. Tafsiri hii inatuwezesha kuwafahamu kundi la marafiki hawa, Asia, Edgar and Kat, ambao wanazamia pamoja nasi katika usomaji, wakiuliza maswali magumu, wakituongoza sehemu moja hadi nyingine, wakituwekea wazi maelezo ya masimulizi magumu, na kutusaidia katika kutujenga kwenye mwamba imara wa imani. Tembelea tovuti hii: www.deepbluekidsbible.com ili uagize nakala yako.

- **Soma Biblia ya Watoto yenye Vielelezo *The DK Children's Illustrated Bible***

Hii inafanya masimulizi maarufu ya Biblia yamvutie msomaji anayeanza; masimulizi yameelezwa kwa wazi na kwa lugha iliyohai. Wazazi wanaweza kujifunza pia wakati wanaposoma na watoto wao. Tembelea tovuti hii: www.dk.com ili kuagiza Biblia ya Watoto yenye Vielelezo.

- **Soma Biblia iitwayo *My First Message* yaani 'Ujumbe Wangu wa Kwanza'**

Hili ni toleo la watoto la ile Biblia iliyoongezewa maelezo ambayo inanunuliwa sana iitwayo *The Message* ya Eugene Peterson, mchungaji na mwalimu, ambaye anafanya lugha ya asili ya biblia ieleweke kwa wazi kwa msomaji wa siku hizi kwa njia ya kubadilisha maandiko kwa kutumia lugha ya kisasa. Tembelea tovuti hii: www.messagebible.com ili kuagiza nakala yako.

2. Soma Biblia kwa Uchangamfu

Watoto huondoa fadhaa za wazazi. Tunapofurahi, wao nao hushiriki furaha yetu. Kusoma Biblia ni tendo la kiroho ambalo linatuwezesha kuyatajirisha kiroho maisha yetu pamoja na watoto wetu. Tuna fursa inayotokea mara moja tu katika maisha yote ya kuwasaidia kulijua Neno la Mungu lililovuviwa na habari zinazookoa. Anza na habari za uumabaji katika Kitabu cha Mwanzo. Agano la Kale lina baadhi ya habari nzuri sana kuliko nyingine katika Biblia yote. Soma habari za mapambano na furaha na safari za ajabu na kuburudisha. Utashangazwa na habari za kuvuka Bahari ya Shamu, uaminifu wa Ruthu, Daudi akisimama mbele ya Goliati na ujasiri wa Esta. Acha Yesu abadilshe maisha yetu kwa miujiza na huruma zake.

3. Fanyeni Zamu ya Kusoma Mara kwa Mara

Mpeane changamoto ya kusimulia kile mlichokisoma. Anzeni kujifunza majina ya vitabu vya Biblia pamoja na mifano na masimulizi mbalimbali. Uvifahamu vitabu kimoja kimoja na jitahidi kupata picha ya jumla na jinsi vitabu hivi vinavyohusiana.

4. Waonyeshe Jinsi Biblia ilivyofanana na Maisha Halisi

Yesu anatueleza katika Luka 6 kuhusu njia za kuisha na kupenda, kusamehe na kujali wengine. Katika Injili ya Mathayo, Yesu anatueleza hatua kwa hatua namna ya kusameheana. Biblia inatupa masimulizi ya maisha halisi na majibu halisi ili tuweze kuujenga ufalme wa Mungu wakati wote tunapoishi. Nyaraka za mitume zinatueleza

namna ya kutunzana na kufuata njia ya Yesu. Uwe na watoto wako wakati wa kulala na uwasomee simulizi moja kila wanapolala usiku. Eleza jinsi habari inavyohusiana na maisha halisi au jinsi isivyohusiana na maisha. Waulize kwa jinsi gani mafundisho ya Biblia yanatusaidia kujenga maisha bora zaidi ulimwenguni na kutufanya tuwe watu bora zaidi. Hizi ni habari za Mungu tulizopewa ili kutuonyesha jinsi Mungu anavyoleta matumaini, uponyaji na upendo. Habari za huzuni zina mwisho wenye furaha. Habari za furaha zinakamilishwa na wajibu. Sisi ni watu wa Mungu, tuliopendwa na kuthaminiwa na Mungu. Wakati mwingine, masimulizi hayatuelezi kile tunachopenda kusikia. Kama ndivyo, basi nini anachotufundisha Mungu? Kama hujui kitu, sema, "sijui kwa nini jambo hili limetokea katika habari hii?" Kisha sema, "Unawaza nini?" Watoto wako watakufundisha, na mtaendelea kukua pamoja katika imani.

5. Soma na Elezea Tena
Chagua habari uipendayo ya Biblia au kifungu na usome vifungu vinavyotangulia na kisha vinavyofuata. Uliza maswali: Ni nini mwandishi anataka tufahamu? Ni jambo gani linatuhusu mimi na wewe katika habari hii? Ungejisikiaje kama ungekuwa katika tukio husika? Je unasikia harufu, unapapasa, unaona na kuhisi nini? Kama ungekuwa na uwezo wa kubadili mwisho wa simulizi hili, ni kitu gani ungekibadili? Je unaweza kuieleza vipi habari hii kwa kutumia maneno yako mwenyewe? Mwishoni mnapomaliza kusoma, muulize mtoto wako: 1) Soma la leo linatueleza nini kuhusu Mungu? 2) Tumejifunza nini kuhusu namna ya kuwatendea watu wengine? na 3) tumejifunza nini kuhusu familia yetu na jinsi inavyotupasa kuishi?

6. Chagua muda na mahali na kisha anza
Kila siku someni mahali pamoja na muda uleule. Wakati wa kulala ni muda mzuri kusoma, lakini fanya lile lililo jema zaidi kwa familia yako na kwako pia. Unaweza kujaribu kusoma injili yote pamoja na watoto kama vile Injili ya Luka ili kujifunza zaidi maisha ya Yesu. Kisha jaribu kusoma Kitabu cha Matendo ili kujifunza jinsi Kanisa lilivyoanza. Fanya maombi na shukrani ili maisha yabadilishwe na yawe yaliyofungiwa nanga katika Neno Takatifu la Mungu.

7. Tunza jarida la shukrani
Kila mara unapomaliza kusoma Biblia, andika daftari lako la kumbukumbu ambalo ndilo litakuwa jarida lako la shukrani kuhusu mambo matatu ambayo yamekufanya ujae shukrani. Hesabu baraka na ushukuru.

8. Toa nafasi ya kuzungumza
Je watoto wako wanawezaje kuzitumia habari hizi katika maisha yao? Kwa mfano, kama binti yako unahuzuni kwa sababu alitendewa vibaya na mwanafunzi mwenzake, katika kipindi chako cha Biblia inaweza kuamua kutafuta habari za upendo (Mathayo 22:34-46), msamaha (Luka 15:1-3, 11-32), kusaidiana (Luka 10:25-37 na urafiki (Luka 19:1-10). Siyo lazima uwe na majibu yote. Kusoma habari za Biblia kutatoa uwanja uliyosalama

wa mazungumzo. Baadaye, mtoto wako anaweza kusema kwa yule mwanafunzi mwenzake, “Sijua kwa nini ulinishusha namna ile. Mimi nataka tuwe marafiki.”

9. Weka Malengo
Majira ya Kwaresma na Maajilio (vipindi kabla ya Krismasi na Pasaka) mara nyingi hutengwa kama nyakati za kujitoa kwa makusudi ili kumjua Mungu akitenda kazi katika maisha yetu. Amua kusoma pamoja na watoto wako kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi kila juma wakati wa majira ya Kwaresma na Maajilio. Pumzika siku ya Jumapili ili kusikiliza Biblia ikisomwa kanisani.

Uchaguzi zaidi wa Kusoma kwa Kina zaidi

1. Soma Biblia ya Mwaka Mmoja
Biblia ya Mwaka Mmoja ina masomo yaliyochaguliwa toka kwenye Biblia kwa ajili ya kila siku, ikitumia masomo kutoka Agano la Kale na Agano Jipya. Hii ni njia bora zaidi ya kumsaidia mtoto wako kupata uzoefu wa kusoma Biblia mara kwa mara kwa kadri anavyoendela kukua. Katika kila hitimisho la somo, jiulize mwenywe: 1) Masomo ya leo yananifundisha nini kuhusu Mungu? 2) najifunza nini kuhusu watu wengine? 3) Yananifundisha kitu gani kuhusu maisha yangu mwenyewe? Tafakari maswali haya peke yako, au na rafiki au kikundi. Tumia *Google* kutafuta: Biblia ya Mwaka Mmoja ili pia upate kuchagua njia nyingine zaidi zinazopatikana kwenye mtandao wa *Amazon.com*

2. Tumia nguvu ya teknolojia na kupakuwa kimtandao Biblia bila
Watoto ni wapenzi wa mfumo wa digitali na hupenda teknologia. Jaribu kupakuwa Biblia kwenye mtandao na kuiingiza kwenye *iPad*, *iPhone*, *Kindle* au *Nook*. Uwe na Biblia yako wakati wote. Mitandao ya *YouVersion.com* na *.bible.com* inatoa taratibu nyingi za usomaji wa Biblia kwa njia ya kusoma Biblia kwa mwaka mmoja huku ikikupa utararibu wa kukuwezesha kujifunza masomo ya imani, upendo na mambo mengine. Tovuti hizi pia zina vipakuzi kwa ajili ya simu za kiganjani kama vile *smart phone*, *iPad*, *Blackberry* na simu za *Android* [kama vile *Sumsung Galaxy Appeal*]. Tovuti ya *Oneyearbibleonline.com* inatoa mpango wa usomaji ambao umegawanywa katika masomo ya kila siku yakiwa na kifungu kutoka Agano la Kale, Agano Jipya, Zaburi, na Mithali. Tovuti ya *Biblegateway.com* ina Biblia nzuri nyepesi kufunguka tena yenye njia nyingi za kukuwezesha kupata unachokitaka. Tovuti nyingine ni *Bibleresources.bible.com* hii ina mambo mengi mazuri. Tovuti za *Amazon.com*, *Zondervan.com*, na *BN.com* zinatoa Biblia za aina mbalimbali na vipakuzi kwa ajili ya simu za kiganjani

na vifaa vya kusomea kama *Kindles*, *Nook Readers*, *Smart phones*, *Blackberry*, simu za *Android*, pia Biblia iliyoigizwa kwa Sauti ya *NIV* na *CD*

3. Sikiliza Biblia

Kuna vifaa vingi vinavyoweza kukuwezesha kusikiliza Biblia unapoendesha gari, ukielekea shuleni, unapotembea na mbwa, unaposafiri, unapofanya kazi za sanaa au mikono au umepumzika nyumbani au kitandani. Hili ni jambo jema sana kwa wale wenye kawaida ya kusikiliza zaidi kuliko kusoma. Unaweza kusikiliza Biblia katika tafsiri mbalimbali kwa njia na programu za kimtandao kama hizi: *Audio.com*/ Bible, listenersbible.com, BibleGateway.com, *YouVersion*.com or www.faithcomesthroughhearing.com. *Faith Comes through Hearing* ambazo zinakupa programu za kusikiliza Biblia katika lugha 692. Unaweza kusikiliza Agano Jipya lote kwa dakika 28 kila siku kwa siku 40.

4. Kukariri Maandiko

Kikariri Maandiko ni njia kuu ya kukuza imani yako na kuongeza ufahamu wako wa Biblia. Tunapokariri kitu, tunaweza kukikumbuka, tunaporudia kukisema kitu kile kile basi hali hiyo inatuwezesha kuwaza, kufanya maamuzi na kueleza yale tunayoyaamini. Kukariri Biblia husaidia kutujenga katika tabia na utu. Pia kuna tovuti iitwayo *bibleminded* ambayo inakuwezesha kukariri vifungu wewe mwenyewe au kwa kufuata njia moja wapo kati ya kadhaa zilizowekwa. Tunashauri usome sura moja ya Biblia kwa siku na kuwekea alama kifungu kimoja cha kukariri. Kiandike kufungu kwenye karatasi au kadi unayoitumia kuwekea alama kwenye Biblia. Tumia dakika kadhaa ukijaribu kukariri hicho kifungu. Chukua karatasi hiyo uwe nayo, fanya mazoezi ya kurudiarudia kusema kifungu kwa siku nzima. Mwisho wa siku, utakuwa umeshakikariri kifungu husika. Vile vifungu uvipendavyo vipitiepitie aghalabu mara moja kwa wiki.

5. Soma Injili ya Luka na Kitabu cha Matendo

Ikiwa kusoma sehemu kubwa ya Biblia ni jambo gumu kwenu, anza polepole. Soma Luka, injili moja iliyo na habari nyingi za maisha ya Yesu na huduma yake na imejaa mifano mikuu. Jambo hili litakupa utangulizi wa maisha ya Yesu. Kitabu cha Matendo kitakufundisha jinsi Wakristo wa mwanzo walivyoanza kueneza ujumbe wa upendo wa Yesu.

6. Fanya Changamoto ya Biblia kwa Mzazi na Mtoto au Changamoto ya Biblia kwa Familia wakati wa Kwaresma

Jitoe kusoma Biblia ya watoto pamoja na motto wako wakati wa siku 40 za Kwaresma na ualike familia nyingine kujiunga nanyi. Mkutane pamoja siku za michezo na kujadili

Biblia pia. Kutana na wazazi wengine ili kuwashirikisha uzoefu wako na wewe kujifunza kutoka kwao.

7. Tumia mitindo mbalimbali ya kujifunza
Kabla watoto hawajawa na mitindo mbalimbali ya kujifunza, kuyakabili maandiko kwa kutumia njia mbalimbali inaweza kuwasaidia. Wale wanaojifunza zaidi wakiona hunufaika wakitazama masimulizi ya Biblia. Furahia masimulizi yaitwayo. *Veggie Tales,* yaani 'Hadithi Mboga' au masimulizi uyapendayo ya Bibia kwenye mtandao wa *youtube*. Wale wanaojifunza zaidi kwa kutenda hufurahia kujifunza kwa kutenda. Tafuta kifungu cha Biblia kinachopendwa, kata neno moja moja ili kuunda chemsha bongo. Wale ambao hujifunza zaidi kwa kusikia watafurahi kusikia Neno likisomwa mbele yao. Jizoeze njia mbalimbali za kujifunza Biblia.

8. Mshirikishe Mwingine furaha yako ya kusoma Biblia
Kama umefurahia na kunufaika na usomaji wa Biblia kwa utaratibu wa kila siku, mshirikishe rafiki au mmoja katika familia kuhusu uzoefu ulio upata. Unaweza kununua Biblia kama zawadi kwa mtu huyo. Waambie kuhusu Changamoto ya Biblia, au waombe wakuruhusu uwaandikishe kuwa washiriki wa usomaji wa Biblia. Amua kusoma tena Biblia pamoja na watu hao na kukutana nao mara kwa mara ili kushirikishana mawazo na uzoefu. Jambo hili litakuza uhusiano kati yenu na uhusiano wenu na Mungu.

Shuhuda

Kwa kawaida mimi hutafuta njia za kufanya mambo pamoja tukiwa kama familia. Mwanangu, Trey, anatakiwa kusoma kwa dakika 20 kila jioni. Wakati mwingine jambo hili ni gumu kwake. Anapenda vitabu vya picha na nilijua ataipenda Biblia iitwayo *The Spark Story Bible*, yaani 'Biblia ya Masimulizi ya Mvuto'. Hii ilikukwa fursa ya kuuwa ndege wawili kwa jiwe moja – kujiunga na Changamoto ya Biblia na kukidhi matakwa ya Trey ya kujisomea. Nilirudi nyumbani usiku ule nikiwa na matazamio makubwa na nikatangaza kuwa tutakuwa tukisoma toleo la Biblia la *Sparks Story Bible* kwa dakika 20 kila siku usiku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kwa majuma nane. Mara nyingi huwa tunazidisha zile dakika 20 zilizopangwa. Kwa kasi hii tungeweza kumaliza Biblia yote kabla ya yale majuma yetu nane hayajaisha. Mara kwa mara Trey huandisha taarifa yake ya maendeleo ya usomaji mara baada ya kumaliza kusoma kila siku na huweka kumbukumbu ya dakika na kurasa alizosoma. – **Karen, mzazi**

Napenda kusoma Biblia. Napenda kujifunza jinsi Mungu anavyojifunua mwenyewe kupitia Maandiko. Zaidi ya yote napenda kusoma Neno pamoja na wengine na kutazama jinsi Mungu anavyojifunua kwao pia. wajukuu wangu wenye umri wa miaka mitano walitumia muda mwingi katika juma wakati wa mapumziko yetu ya kiangazi wakishangaa, wakitafakari na kujifunza miujiza ya Mungu ya jinsi Musa alivyowaongoza

Waisraeli kutoka utumwani na kifungoni hadi kwenye uhuru. Wajukuu hawa walijifunza kwamba Mungu hutusaidia kufanya maamuzi mema, hasa katika wakati mgumu. Kwa pamoja, wote tuligundua ukuu wa wakovu wa Mungu katika Neno Takatifu la Mungu. Nitalithamini milele. – **Hillary, babu**

Napenda kusoma Biblia. Inasisimua. Kwa kawaida nasema, Hapana! Wakati tunapotakiwa kwenda kulala (wakati masimulizi ya Biblia yameisha). Sisi huandika makala za shukrani baada ya kusoma Biblia. Napenda kuandika vitu vile ninavyovifurahia. – **Teddy, miaka 7**

Nilizoea kutokujua mambo mengi kuhusu Biblia. Nilidhani inahusu sheria tupu. Pia niliwaza kuwa ilihusu mambo ya heri tu. Kwamba Yesu alikuja duniani ili kuwashukuru watu. Ni jambo jema kujifunza zaidi kuhusu Mungu na Yesu. Ni jambo gumu kwa vijana kujifunza mambo ya Mungu pasipo kusoma Biblia. – **Margaret, miaka 9**

Unaposoma Biblia unaanza kuuona ulimwengu katika naman mpya. Ua linageuka kuwa muujiza. – **Caroline, miaka 11**

Tunatazamia kuwa umepata uzoefu mkubwa katika Changamoto ya Biblia kwa Mzazi na Mtoto. Ikiwa jambo hili la kiroho limegusa moyo wako na kukupa chakula cha kiroho, nakualika uchangie Kituo cha Masomo ya Biblia ili kusaidia kukuza Changamoto ya Biblia ili wengine wanufaike na usomaji wa Neno la Mungu kila siku na kushiriki katika Changamoto ya Biblia. Sadaka yako inaweza kutolewa kwa "*St. Thomas Episcopal Church*" ukieleza ni kwa ajili ya "*The CBS*" na uitume kwenda *St. Thomas Episcopal Church, P.O. Box 247, Fort Washington, Pennsylvania, 19034*

Nuru na upendo wa Mungu vikuangazie kila siku,

Mch. Marek P. Zabriskie na Mch. Hillary West

Mchungaji Kiongozi na Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Mt. Thomasi la Fort Washington, Pennsylvania,
Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia.
Ili kujiunga na Changamoto ya Biblia kwa Mzazi na Mtoto, tafadhari nitumie barua pepe kwa anuani hii: *mzabriskie@stthomashwhitemarsh.org*